



Kila mtu mwenye umri wa miaka 16 na zaidi anaweza kupata chanjo ya COVID-19 BILA MALIPO hivi sasa!

Chanjo za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi.

Chanjo za COVID-19 zinatuseaidia kurejelea maisha yetu ya kawaida. Manufaa ya kupata chanjo yanazidi sana hatari za kupata virusi. Watu wengi hupata athari nyepesi au za wastani, kama vile uchungu kwenye mkono. Chanjo zina ufanisi wa juu katika kuzuia maradhi makali, kulazwa hospitalini na kifo kutokana na COVID-19.



Ili kupata mtoa huduma wa chanjo karibu nawe, tembelea vaccinefinder.org. Unaweza kujiandikisha kwa miadi mtandaoni au kupitia simu. Baadhi ya kliniki zinazotoa chanjo zitakubali kuingia bila miadi au ujiandikishaji katika eneo lao. **Nafasi za miadi zinaweza kujaa haraka. Inaweza kuchukua majaribio kadhaa kupata miadi.**

- **Chanjo inatolewa BILA MALIPO kwa kila mtu.** SI LAZIMA uwe na bima ya afya, uwe raia au mkazi wa Marekani, au uwe na nambari ya ustawi wa jamii. Watoa chanjo hawatozi maelezo yoyote yako kwa idara ya uhamiaji au utekelezaji wa sheria.
- Lazima ulete kitu ambacho kina jina lako (kama vile kitambulisho cha picha, bili ya matumizi, au barua iliyosainiwa kutoka kwa mtu anayethibitisha utambulisho wako).
- Ikiwa huna kompyuta au huwezi kupata Intaneti, omba mtu unayemwamini akusaidie kujiandikisha kwa miadi.
- Unaweza kutaka kumjulisha mtoa chanjo kabla ya wakati ikiwa utahitaji mipango maalum (kama vile usaidizi wa lugha au kiti cha magurudumu).

Ikiwa una maswali kuhusu chanjo ya COVID-19, tembelea coronavirus.utah.gov/vaccine au upige Simu ya Dharura ya COVID-19 kupitia **1-800-456-7707**.